Msilifanye kaburi langu kuwa sikukuu, wala nyumba zenu kuwa makaburi, na nitakieni rehma, kwani dua zenu hunifikia popote mlipo

Kutoka kwa Ally bin Husein: "Yakwamba yeye aliona mtu mmoja anakuja toka katika kiupenyo kidogo kilikuwa katika kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- anaingia na anaomba hapo, akamkataza, na akasema: Hivi nikusimulieni hadithi niliyoisikia toka kwa baba yangu toka kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Msilifanye kaburi langu kuwa sikukuu, wala nyumba zenu kuwa makaburi, na nitakieni rehma, kwani dua zenu hunifikia popote mlipo".
[Ni sahihi kwa njia zake na ushahidi wake] [Imepokelewa na Ibn Abii Shaybah]

Anatueleza Ally bin Husein -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- yakwamba yeye alimuona mtu mmoja akimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kaburi la Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake-, nakuwa yeye alimkataza juu ya hilo kwa ushahidi wa hadithi ya Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- ambayo limekuja ndani yake katazo la kulifanyia mazoea kaburi lake kwa ziara, na katazo la kuzitelekeza nyumba kwa kutokuwa na ibada ya Mwenyezi Mungu ndani yake na dhikri, na kuifananisha kwake na kaburi, na akaeleza kuwa salamu ya muislamu itamfikia yeye -Rehema na Amani ziwe juu yake- mahala popote atakapokuwa muislamu.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3346